JAMHURI YA MUUANGANO WA TANZANIA

MTIHANI WA AWALI WA UTAMILIFU

KISWAHILI KIDATO CHA NNE

Muda saa 2:30 **March, 2025**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, na B, na maswali mawili (2) kutoka sehemu C ambapo swali la tisa (9) ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama kumi na sita (16) sehemu B alama hamsini na nne (54) na sehemu C alama thelathini (30)
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani
7. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia

LUSAELIMU.COM

SEHEMU A (Alama 16)

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu sahihi

(i) Maneno yafuatayo yana maana Zaidi ya moja isipokuwa

A. Ua
B. Mbuzi
C. Kata
D. Nyau
E. Paa

(ii) Kipi ni kipengele kinachohusu mjengo wa kazi ya fasihi

A. Mtindo
B. Muundo
C. Mandhari
D. Wahusika
E. Lugha

(iii) Pande mbili zinazohusika katika lugha ya maandishi ni zipi?

A. Mwandishi na msikilizaji
B. Msikilizaji na msomaji
C. Msilizaji na mzungumzaji
D. Msomaji na msimuliaji
E. Msomaji na mwandishi

(iv) Njia ipi hutunza sauti pamoja na vidokezo vyake katika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kati ya hizi?

A. Maandishi
B. Mikanda ya filamu

C. Mitandao
D. Kinasa sauti
E. Masimulizi

(v) Kikundi cha maneno kinachoonesha jamii lililotendwa na mtenda katika sentensi hujulikanaje?

A. Chagizo
B. Kitenzi
C. Kivumishi
D. Shamirisho
E. Nomino

(vi) Tungo ipi ina kiambishi rejeshi kati ya hizi?

A. Anaondoka
B. Ameondoka
C. Aliondoshwa
D. Amejiondoa
E. Ameondokewa

(vii) Kushindana na mtu aliyekuzidi kwa kila hali si busara "Methali zifuatazo zinashabihisha kauli hii isipokuwa

A. Mwenyepesa si mwenzio
B. Nazi haishindani na jiwe
C. Chanda chema huvishwa pete
D. Mwenye nguvu mpishe
E. Maji yakija kasi yapishe

(viii) Kiangazi kiliunguza kikaunguza ……hatimae mwaka elfu moja mia tisa hamsini na sita mvua zikaanza ijapokuwa kwa mazingo"

Usimulizi huu ni aina gani ya hadidhi?

A. Visasili
B. Vigano
C. Soga
D. Ngano
E. Tarihi

(ix) Papai limeiva nyumbani lakini nashindwa kulila kauli hii inawakilisha aina gani ya semi?

A. Methali
B. Mizungu
C. Nahau
D. Vitendawili
E. Misemo

(x) Msaada wako umenifaa sana. Asante! Neno "Asante" ni aina gani ya neno?

A. Nomino
B. Kivumishi
C. Kielezi
D. Kielezi
E. Kihisishi

2. Oanisha maana ya dhana katika orodha A na dhana zinazohusika kutoka orodha B kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi

Orodha A	Orodha B
i. Sehemu ya neno inayotamkwa mara moja kwa pamoja kama fungu moja la sauti ii. Utamkaji wa maneno unaozingatia kanuni za sauti ya Lugha iii. Nguvu inayotumika kutamka sehemu Fulani ya neno iv. Vitamkwa vinavyotamkwa na binadamu kwa ktumia viungo sauti v. Jinsi mtu anavyotamka maneno ya lugha vi. Kupanda na kushuka kwa mawimbi sauti	A. Lafudhi B. Matamshi C. Kiimbo D. Mkazo E. Silabi F. Lugha G. Sauti

Orodha A	i	ii	iii	iv	v	Vi
Orodha B						

3. Tumia kiambishi “KA” kuonesha matukio 10

4. Yapange maneno yafuatayo kama yanavyoonekana katika kamusi kisha eleza maana ya kila neno kwa kutoa mfano mmoja wa sentensi

A

. Falsafa

B. Barizi

C. Anuwai

D. Barubaru

E. Kinda

F. Ajuza

G. Fanusi

H. Ghaibu

I. Goigoi

J. Kinanda

5. (a) Katika kila sentensi, andika neno moja lenye maana sawa na maelezo ya sentensi husika

i. Mtu anaechunguza uhalifu

ii. Ng’ombe dume aliyehasiwa

iii. Chombo cha usafiri kinachopita juu ya vyuma

iv. Mti unaozaa matunda yanayotengeneza kinywaji cha kahawa

v. Sehemu ndogo ya nchi iliyochongoka na kuzungukwa na bahari katika sehemu zake tatu

(b) “Mofimu huru zina hadhi ya neno”. Fafanua usemi huu kwa kutumia sentensi nane (8) tofauti.

i.

ii.

iii.

iv.

6. Toa maana tano tofauti za neno “kibao” kisha tunga sentensi moja kwa kila maana uliyotoa.

7. Tunga tungo zenye vipashio vifuatavyo

(a) Nomino + kishazi tegemezi + Prediketa + Shamirisho

(b) Kiimakapa + Prediketa + Chagizo

(c) Kirai nomino + Kishazi huru + Kishazi tegemezi

(d) Nomino + Kitenzi + Kielezi

8. Jifanye wewe ni Gulamali Banji anayeishi mtaa wa Tandamti gerezani Kariakoo na unataka kuuza gari yako aina ya CARINA. Andika Tangazo kwenye gazeti la mwananchi.

SEHEMU C (Alama 30)

9. “Fasihi ni nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii” Thibitisha kauli hii kwa kutumia diwani mbili ulizosoma.

10. “Mapenzi ya dhati huleta faraja miongoni mwa wanajamii” Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila riwaya kati ya riwaya mbili ulizosoma.

11. Kwa kutoa hoja mbili na mifano eleza namna jina la kitabu linavyosadifu yaliyomo katika tamthiliya mbili ulizosoma.

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

WASAKATONGE - M.S Khatibu (DUP)
MALENGA WAPYA - TAKILUKI
(DUP) MASHAIRI YA CHEKA CHEKA -T A Mvungi
(EPD. LTD)

RIWAYA

TAKADINI - Ben J.
Harson (M A) WATOTO WA MAMA NTILIE - E.
Mbogo (H.P) JOKA LA MDIMU - AJ Safari

TAMTHILIYA

ORODHA - Steve
Reynolds (MA) NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE-
E. Semzaba
KILIO CHETU - Medical Aid Foundation